Tangazo la Serikali Na. 551 la tarehe 28/9/2018

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA 272)

---

**AGIZO Namba 2018 - .......**

---

*(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (d))*

AGIZO LA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SONGEA ("SONGEA WSSA"), LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2018

Kichwa cha Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea ("Songea WSSA"), (la Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), la Mwaka 2018.

Tarehe ya Kuanza

2. Agizo hili litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Oktoba 2018.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Songea WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Agizo hili.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) Ifikapo tarehe 31 Januari 2019 au kabla, Songea WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Agizo hili.

(b) Songea WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Agizo hili.

(c) Songea WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Agizo hili.

(d) Songea WSSA, kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa.

(e) Songea WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na

EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Songea WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Songea WSSA katika siku zijazo.

Agizo Na. 27-014 la tarehe 1 Agosti 2014

Agizo hili linatengua Agizo Na. 27-014 la tarehe 1 Agosti 2014 katika maeneo yanayohudumiwa na Songea WSSA.

## MAJEDWALI

### JEDWALI LA KWANZA: BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ mita ya ujazo)

| Kundi la Wateja | Kundi la matumizi (mita za ujazo) | Bei za Ssasa | Bei iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 0-10 | 895 | 1,000 | 1,110 | 1,155 |
| | 10 <25 | 970 | 1,100 | 1,200 | 1,250 |
| | >25 | 1,000 | 1,150 | 1,240 | 1,290 |
| Biashara | 0-10 | 1,000 | 1,150 | 1,240 | 1,290 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | > 10 | 1,075 | 1,200 | 1,330 | 1,385 |
| Taasisi | 0-20 | 925 | 1,060 | 1,145 | 1,190 |
| | >20 | 1,000 | 1,150 | 1,240 | 1,290 |
| Viwanda | 0-10 | 1,000 | 1,150 | 1,240 | 1,290 |
| | >10 | 1,075 | 1,250 | 1,330 | 1,385 |
| Magati | | 500 | 500 | 500 | 500 |

Jedwali Namba 1(b): Tozo ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Huduma (Shilingi/Mwezi)

| Kundi la Wateja | Tozo za Sasa | Tozo iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 3,000 | HAIJAIDHINISHWA | | |
| Biashara | 4,000 | | | |
| Taasisi | 3,500 | | | |
| Viwanda | 4,500 | | | |

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/unganisho)

| Kundi la Wateja | Ada za Sasa | Ada iliyoidhinishwa |
|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19-2020/21 |
| Majumbani | Asilimia ishirini ya gharama ya vifaa | Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013 |
| Biashara | | |
| Taasisi | | |
| Viwanda | | |

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 15,000 | 18,000 | 20,000 | 22,000 |
| Biashara | 15,000 | 18,000 | 20,000 | 22,000 |
| Taasisi | 15,000 | 18,000 | 20,000 | 22,000 |
| Viwanda | 15,000 | 18,000 | 20,000 | 22,000 |

Jedwali Namba 1(e): Bei ya sasa na Iliyoidhinishwa ya Huduma ya Majitaka (Shilingi/ Mwezi)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 355 | 400 | 400 | 400 |
| Biashara | 625 | 650 | 675 | 700 |
| Taasisi | 600 | 625 | 650 | 675 |
| Viwanda | 630 | 650 | 675 | 700 |

Jedwali Namba 1(f): Tozo ya sasa na Iliyoidhinishwa ya Magari ya Majitaka (Shilingi/ Safari)

| Kundi la Wateja | Umbali (Kilometa) | Tozo ya Sasa | Tozo Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Wateja wote | 0-10 | 60,000 | 65,000 | 70,000 | 75,000 |
| | 10<-20 | 70,000 | 75,000 | 80,000 | 85,000 |
| | 20<-30 | 80,000 | 85,000 | 90,000 | 95,000 |

JEDWALI LA PILI

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA

| Maelezo | Gharama (TZS/Millions) | | |
|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| A: Miradi Mipya | | | |
| Kuongeza mtandao wa maji kwa kilometa 78 kutoka kilometa440 (Juni 2018 ) mpaka kilometa 518 (2020/21) katika maeneo ya Mshangano, Ruhuwiko, Matarawe, Seedfarm, Lizaboni, Mjimwema, Making'inda and Mkuzo | 113.0 | 200.3 | 164.2 |
| Kununua Dira za maji 500 za malipo ya kabla za DN15 (Prepaid Water Meters) | 45.0 | 45.0 | 60.0 |
| Kununua na kuweka Dira za maji 4000 za DN15. | 90.0 | 153.0 | 117.0 |
| Kununua Simu 50 za kusomea dira za maji (new smart phones for meter reading) | 12.0 | 4.0 | 4.0 |
| Kununua kifaa cha kuchanganyia chroline( automatic online chlorine dosing machine) | 0.0 | 20.4 | 0.0 |
| Kuongeza mtandao wa Majitaka kwa kilometa 7.5 katika maeneo ya Majengo and Misufini | 29.21 | 30.4 | 31.7 |
| Jumla ya Miradi mipya | 289.21 | 453.11 | 376.85 |
| B: Ukarabati | | | |
| Ukarabati wa jengo la mgahawa ili litumike kama kituo cha mauzo na kuongeza ofisi za wafanyakazi. | 24.36 | - | - |
| Ukarabati ya gari aina ya ISUZU - | - | 34.95 | - |

| | | | |
|---|---|---|---|
| STJ 9427 | | | |
| Ukarabati ya gari aina ya FORD RANGER -SU 38783 | - | 2.30 | - |
| Kununua pikipiki 5 | 4.60 | 6.90 | - |
| Jumla ya Ukarabati | 28.96 | 44.15 | - |
| JUMLA YOTE | 318.17 | 497.26 | 376.85 |

JEDWALI LA TATU
VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2020/21)

| Maelezo | Uniti | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Idadi ya wateja wapya wa maji safi | Na | 1,425 | 1,425 | 1,425 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | % | 22 | 21 | 20 |
| Wateja wenye Dira | % | 100 | 100 | 100 |
| Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato | % | 90 | 92 | 95 |

Dodoma
30 Agosti 2018

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi Mkuu*